

# CHUO KIKUU CHA SOKOINE CHA KILIMO

# SUA

## MATUKIO YA MWEZI OKTOBA HADI DISEMBA, 2020





**Warioba aipongeza Menejimenti ya SUA kwa kazi kubwa wanayofanya** Uk. 3



**Wahitimu SUA watakiwa kutambua kuwa hakuna kazi ya maisha bali kuna fursa za maisha.** Uk. 13

**"ARDHI NI HAZINA"**

# SUA KUENDELEZA USHIRIKIANO NA WAKULIMA KATIKA KILIMO CHA IKOLOJIA

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) kimesema kinaendelea kushirikiana na Wakulima na Wadau wengine wa kilimo katika kuhakikisha Kilimo Ikolojia (AGROECOLOGY) kinakuwa endelevu na chenye tija na kinachozingatia utunzaji wa mazingira.

Hayo yamebainishwa na Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Utawala na Fedha kutoka SUA, Prof. Amandus Muhairwa kwa niaba ya Makamu Mkuu wa Chuo hicho, wakati akifungua Mdahalo wa Siku ya Chakula Duniani ambao umefanyika siku ya Ijumaa tarehe 16 Oktoba, 2020 chuoni hapo kwenye Kampasi ya Edward Moringe mjini Morogoro.

Amesema kuwa wao kama Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) wanafanya jitihada mbalimbali kuhakikisha Kilimo hicho cha Ikolojia kinawafikia Watanzania hususani Wakulima ili kuepukana na Changamoto mbalimbali zinazosababishwa na kilimo cha zamani ambacho kwa kiasi kikubwa kimechangia uharibifu wa mazingira.



*Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (Utawala na fedha) Prof. Amandus Muhairwa akiongea na waandishi wa habari mara baada ya kumalizika kwa mdahalo wa Siku ya Chakula Duniani.*

“Na katika kuhakikisha Kilimo Ikolojia kinakuwa endelevu Chuo kimeanzisha Shahada ya Kilimo cha Ikolojia ili kuweza kuzalisha wataalam watakaoendeleza kilimo hicho” amesema Prof. Muhairwa

Awali akizungumza katika Mdahalo huo Cecile Frobert kutoka

Ubalozi wa Ufaransa amesema Ufaransa na wadau wengine wa kilimo inaendelea na juhudi za kuendeleza Kilimo Ikolojia ambacho kinasaidia kukifanya kilimo kuwa endelevu huku akitoa wito wa kuepukana na kilimo cha mazoea cha kutumia madawa ambacho kina madhara kiafya.

Kwa upande wake Jasmien De Winne kutoka Ubalozi wa Ubeligiji amesema vipaumbele vya nchi hiyo ni kufanya shughuli endelevu za kilimo zinazolenga kuboresha maisha ya watu na kuwataka wadau wa Kilimo kujifunza kuendeleza kilimo ambacho hakitaharibu mazingira na kitakuwa na faida kwa kizazi cha sasa na kijacho.

Inatoka Uk. 1

Akizungumzia mdahalo huo Mratibu wa Kituo cha Kilimo Ikolojia ambaye pia ni Mkurugenzi wa Taasisi ya Elimu ya Kujiendeleza ICE- SUA Prof. Dismas Mwaseba amesema kwa muda sasa Chuo kimekuwa kikifanya tafiti zinazolenga kumuwezesha mkulima kupata zaidi bila kuharibu mazingira

Kwa upande wao baadhi ya wakulima walioshiriki katika Mdahalo huo akiwemo Msakuzi Idd na Bahati Swalehe kutoka kata ya Mbuyuni kijiji cha Kibwaya kilichopo Morogoro vijijini wamesema tangu walipoanza kutumia Kilimo Ikolojia wameweza kupunguza gharama za kilimo na hivyo kupata faida zaidi.

Akifunga Mdahalo huo kwa niaba ya Makamu Mkuu wa Chuo upande wa Taaluma, Prof. Samwel Kabote aliwashukuru watu wote waliohudhuria Mdahalo huo na kipekee zaidi aliwashukuru wazungumzaji wote na kusema kuwa umekuwa ni Mdahalo wa kuvutia na wa kuelimisha na anaamini kila aliyehudhuria mdahalo huo ameridhishwa na Elimu iliyotolewa.

Mdahalo huo wa siku moja ambao umehusisha wadau kutoka SUA , SAT, RECODA, Wakulima,Wanafunzi pamoja na Wadau wengine wa Kilimo umebeba kauli mbiu isemayo "Kilimo cha Ikolojia kama njia ya kuelekea Mfumo Endelevu wa Chakula".



*Baadhi ya washiriki na wageni waalikwa wakifatilia kwa umakini maelezo yaliyokuwa yakitolewa na wataalamu kuhusiana na Kilimo Ikolojia wakati wa Mdahalo wa siku ya Chakula Duniani uliofanyika Kampasi ya Edward Moringe, SUA , Morogoro.*

# WARIOBA AIPONGEZA MENEJIMENTI YA SUA KWA KAZI KUBWA WANAYOFANYA



*Mkuu wa Chuo cha SUA  Jaji Mstaafu Mhe. Joseph Sinde Warioba (kushoto) akiwa kwenye picha ya pamoja na Makamu Mkuu wa Chuo hicho Prof. Raphael Chibunda wakati wa ziara yake ya siku mbili chuoni hapo mwezi Novemba,2020*

Mkuu wa Chuo Kikuu cha-Sokoine cha Kilimo (SUA) Jaji Mstaafu Mhe. Joseph Sinde Warioba ameipongeza Menejimenti ya Chuo hicho kwa juhudi kubwa wanazofanya katika shughuli mbalimbali za Kilimo na Utafiti zinazokifanya Chuo kuwa bora na cha kuvutia zaidi nchini na Duniani kwa ujumla.

Mhe. Warioba ameyasema hayo siku ya Jumatano Tarehe 18 Novemba, 2020 wakati akiongea na Wandishi wa habari nje ya Jengo la Utawala la Kampasi ya Solomon Mahlangu akikamilisha ziara yake ya siku mbili aliyoanza siku ya Jumanne Tarehe 17 Novemba, 202 kwenye Kampasi ya Edward Moringe Mjini Morogoro.

Amesema kuwa licha ya Changamoto mbalimbali zikiwemo ukosefu wa rasilimali unaoikabili SUA lakini uongozi wa Chuo umeendelea kupambana kuhakikisha unatimiza malengo ya Chuo ya kutoa elimu iliyo bora kwa Wanafunzi lakini pia elimu ya vitendo hususani kwa vijana na wakulima wadogo wadogo wanaokizunguka Chuo na hata maeneo mengine ya Mkoa wa Morogoro na nje ya Mkoa huo.

"Ni kweli tunazo changamoto lakini nimevutiwa sana na jitihada zinazofanywa hapa Chuoni kama vile Tafiti na Miradi mbalimbali kwa mfano ule mradi wa panya ambao wanagundua mabomu na kutibu kifua kikuu. Nimetembelea Mashamba darasa na kwenye vitalu nyumba ambapo vijana wanapewa mafunzo mbalimbali ya kilimo, kwa kweli huu ni msingi mzuri ambao hautasaidia vijana tu bali utabadili mfumo wa kilimo chetu na kuwa wa kisasa zaidi. Niseme tu, kazi inayofanywa na uongozi wa Chuo ni kubwa na inaridhisha" alisema Mhe. Warioba

Awali kabla ya kuanza kwa ziara hiyo Mwenyekiti wa Baraza la Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) Jaji Mstaafu Mhe. Othman Chande alimshukuru Mkuu wa Chuo kwa kuweza kutenga muda wake na kuja kwenye ziara hiyo licha ya majukumu mengi aliyonayo na kumueleza majukumu mbalimbali yaliyotekelezwa na Baraza kwa kipindi chote ambacho hakufanikiwa kuja Chuoni hapo, ikiwemo kusimamia mpango mkakati wa Chuo wa awamu ya nne wa 2016/2021 ambao ulianza kutekelezwa tangu tarehe 1 Julai, 2016.

Mhe. Chande alimweleza Mkuu wa Chuo Baadhi ya mambo mengine yaliyofanywa na Chuoni kama vile uanzishwaji wa Kampasi ya Mizengo Pinda iliyopo Mkoani Katavi, kuidhinisha taarifa ya ukaguzi wa nje, uanzishaji wa miradi mikubwa mfano ule wa Misitu Ujulikanao kama "Reforest Africa" , kusimamia mali za Chuo , Miradi ya maende-

**Inatoka Uk. 3**

leo ikiwa ni pamoja na mapato na matumizi ya fedha na kufanya teuzi mbalimbali.

"Mhe. Mkuu wa Chuo napenda pia kuchukua nafasi hii kwa niaba ya Baraza kuishukuru sana Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ruzuku na fedha za maendeleo inayotoa kwa Chuo na pesa zinazotolewa kwa ajili ya wanafunzi ambazo zinakuja kwa wakati kwani bila fedha hizo Chuo kisingeweza kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi" alisema Mhe. Chande.

Akiongea kwa niaba ya Menejimenti na Jumuiya nzima Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) Prof. Raphael Chibunda alimshukuru Mkuu wa Chuo kwa kuja kutembelea Chuo na kueleza kwa kifupi utekelezaji wa majukumu ya Chuo tangu mara ya mwisho alipotembelea Chuoni hapo.

Prof. Chibunda alimweleza mhe. Warioba Baadhi ya mambo mbalimbali na muhimu yaliyotekelezwa na Chuo kama vile, ujenzi na ukarabati wa miundombinu kama barabara, ujenzi wa Maabara Mtambuka yenye uwezo wa kuchukua Wanafunzi 2400 kwa wakati, Ujenzi na ukarabati wa Karakana kikiwemo kiwanda cha samani cha Vuyisile kilichopo Kampasi ya Solomon Mahlangu, ukarabati wa ofisi za Wafanyakazi, upanuzi wa Hospitali ya SUA, ukarabati wa hosipitali ya Taifa ya Rufaa ya wanyama na uwanzishaji wa Shamba darasa la mfano.

Licha ya changamoto mbalimbali zinazoikabili Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) kama vile upunguvu wa Wafanyakazi katika kada mbalimbali, Prof. Chibunda hakusita kuishukuru Serkali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania chini Mhe. Rais Dkt. John Pombe Magufuli kwa kuendelea kutoa fedha za miradi ya maendeleo ya Chuo na kulipia gharama mbalimbali za uendeshaji wa Chuo.

Prof. Chibunda pia alitumia fursa hiyo kumshukuru Mkuu huyo wa Chuo kwa kufanya teuzi mbaimbali chuoni hapo ambapo alimuhakikishia kuwa watu wote aliowateua anashirikiana nao vizuri na wanatimiza majukumu yao ipasavyo.



*Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) Jaji Mstaafu Mhe. Joseph Sinde Warioba akipata maelezo toka kwa Dkt. Georges Mgode kuhusu shughuli mbalimbali zinazofanywa na idara ya Apopo ikiwemo ufundishaji wa Panya wanaogundua mabomu na Kifua kikuu*

# WANAFUNZI WA MWAKA WA KWANZA WATAKIWA KUSOMA KWA BIDII



*Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) upande wa Taaluma Prof. Maulid Mwatawala akitoa neno wakati wa hafla ya kuwakaribisha Wanafunzi wapya wa SUA iliyofanyika Kampasi ya Solomon Mahlangu, Mazimbu, Morogoro*

Wanafunzi wa mwaka wa kwanza wametakiwa kusoma kwa bidii na kuzingatia masomo yao Chuoni ili kutimiza ndoto walizonazo kwenye maisha yao.

Wito huo umetolewa na Naibu wa Makamu Mkuu wa Chuo Taaluma kutoka Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo SUA Prof. Maulid Mwatawala kwa niaba ya Makamu Mkuu wa Chuo wakati wa kuhitimisha wiki ya kuwakaribisha Wanafunzi na kuyatambua mazingira ya SUA kwa wanafunzi wa mwaka wa masomo 2020/2021 yaliyofanyika Siku ya Ijumaa tarehe 27 Novemba 2020 katika ukumbi wa Freedom Square uliopo Kampasi ya Solomon Mahlangu iliyopo Mazimbu.

Prof. Mwatawala amewataka wanafunzi hao kutumia muda wao vizuri kwenye masomo yao na kujiepusha na vitu ambavyo vitaweza kuwasababishia kufeli, kuhairisha mwaka pamoja na kutoendelea na Chuo.

"Badala ya kusubiri kupambana karibu na mitihani ya mwisho ya muhula ni vizuri kuanza kuzingatia kusoma kwa bidii kuanzia sasa ili kupata wastani wa juu kwenye masomo yenu", alisema Prof. Mwatawala.

Kwa upande wake Mshauri wa Wanafunzi kutoka SUA Bw. Pule Motshabi amewapongeza wanafunzi wa mwaka wa kwanza kwa kuchaguliwa katika Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo SUA na kuwahakikisha kuwa wamefanya chaguo sahihi kukichagua Chuo cha SUA kwani ni Chuo Bora Tanzania na Afrika kwa ujumla.

Naye Rasi wa Ndaki ya Sayansi na Insia kutoka SUA Prof. Samwe-

*Inatoka Uk. 5*

li Kabote amesema kuwa lengo la Chuo kuaanda zoezi ilo ni kuwafanya wanafunzi wajue mazingira ya Chuo, kutambua viongozi wa Chuo na sheria mbalimbali zilizowekwa na Chuo.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Shahada za Awali kutoka SUA Dkt. Nyambilila Amuri amewataka wanafunzi hao kuzingatia masomo yao pamoja na kazi za kitaaluma watakazopewa na kuwa na nidhamu nzuri ili kutimiza malengo waliojiwekea.

“Maisha ya chuo cha SUA yataongozwa na sheria zilizowekwa ili kukuongoza wewe mwanafunzi kufanya vizuri katika masomo yako na kutimiza ndoto zako hivyo ni vizuri kufuata kanuni na taratibu zote zilizowekwa chuoni”, amesema Dkt. Nyambilila.

Aidha Dkt. Nyambilila amewasisitizia wanafunzi kuwa endapo wakutana na changamoto yoyote ni vizuri kuomba ushauri katika ofisi za ushauri ili waweze kusaidiwa badala ya kubaki nazo.

Akitoa salamu za shukrani Makamu wa Serikali ya Wanafunzi Bi. Mary Magoti Kutoka SUA ameishukuru Menejimenti ya Chuo kwa kuandaa zoezi hilo la kuwakaribisha wanafunzi wa mwaka wa kwanza na kuwatambulisha mazingira ya Chuo kwani itawasaidia wanafunzi hao kutokuwa na hofu ya kuwa Chuo cha SUA ni kigumu na badala yake watajiandaa vizuri kwenye masomo yao.

Pia amewahakikisha wanafunzi hao kuwa Serikali ya wanafunzi imejipanga vizuri kushirikiana nao na kuendelea kuwaelekeza taratibu zote za muhimu wanazotakiwa wazifuate ili maisha ya Chuoni hapo yawe mepesi.



# WANAJUMUIYA SUA WAHASWA KUSHIRIKI MICHEZO MARA KWA MARA




*Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) upande wa Utawala na Fedha Prof. Amandus Muhairwa akitoa neno wakati wa ufunguzi wa mashindano ya ndani ya wafanyakazi maarufu kama Chibunda Cup.*

Wanajumuiya wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) wamehaswa kuwa na mazoea ya kushiriki kwenye michezo mara kwa mara kwani mbali na michezo kuwa sehemu ya furaha na kujenga urafiki lakini pia huimarisha afya ya mwili na kuepuka magonjwa mbalimbali.

Kauli hiyo imetolewa na Naibu Makamu Mkuu wa Chuo (Utawala na Fedha) Prof. Amandus Muhairwa akimuwakilisha Mgeni rasmi ambaye ni Makamu Mkuu wa Chuo wakati wa ufunguzi wa mashindano ya michezo ya ndani ya Wafanyakazi wa SUA maarufu kama "PROFESA CHIBUNDA CUP" inayofanyika kwenye Viwanja vya michezo vya Kampasi Kuu kuanzia tarehe 9 Oktoba hadi tarehe 13 Oktoba, 2020.

"Nichukuwe nafasi hii kuwapongeza waandaaji wa mashindano haya pamoja na washiriki wote waliotenga muda wao na pia niwaombe muendelee na utaratibu huu wa kushiriki michezo wakati wote sio tu mpaka kipindi cha mashindano kama hivi kwani michezo inafaida nyingi sana" alisema Prof. Muhairwa

Prof. Muhairwa pia alitumia nafasi hiyo pia kuwashukuru wawakilishi wa Benki ya CRDB pamoja na NMB kwa sapoti yao kubwa wanayoitoa katika michezo inayofanyika Chuoni hapo hususani kwenye mashindano hayo ya Chibunda Cup.

"Naamini tungeweza kucheza bila uwepo wenu lakini tusingeweza kucheza vizuri kama tunavyocheza sasa na naamini shamra shamra hizi zinachagizwa na uwepo wenu

**Inatoka Uk. 7**

hususani Benki ya CRDB ambao tumekuwa nanyi tangu kuanza kwa mashindano haya, karibuni sana" alisema Prof. Muhairwa

Akiongea kwa niaba ya Benki ya CRDB Bi. Isabela Kitila alikishukuru Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) kwa kuendelea kuiamini Benk hiyo na kuahidi kuendelea kushirikiana nao bega kwa beka katika michezo kila wakati.

Nae Meneja wa NMB kanda ya mashariki Bw. Dismas Prosper alitoa shukurani zake kwa uongozi wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) kwa kuwaalika kuwa miongoni mwa washirika katika mashindano hayo na kuahidi kushiriki kikamilifu katika michezo Chuoni hapo.

"Na mimi ni kama ambavyo wamesema wenzangu waliotangulia kuwa michezo ni furaha, michezo inaburudisha na sisi kama NMB tuna ahidi kutoa ushirikiano wa kutosha na natamani kama ningewaona vijana zaidi wakishiriki kwenye michezo hii kwani mbali na kujenga urafiki na undugu lakini michezo pia ni ajira inayoajiri idadi kubwa ya watu hususani vijana"

Akitoa neon la shukurani Mkurugenzi wa mipango na maendeleo Dkt. Ibrahimu Mjema alimshukuru mgeni rasimi kwa kutenga muda wake kushiriki kwenye ufunguzi huo licha ya kuwa na majukumu mengi.

"Nitumie fursa hii pia kuwashukuru na Wageni wengine waalikwa ikiwewmo Benki ya CRDB na NMB pamoja na Marasi wa Ndaki mbalimbali hapa Chuoni kwani tukio hili ni la kwetu sote Wanajumuiya wa SUA hivyo yatupasa kushiriki kikamilifu na kufurahia kwa pamoja"

Wakati huohuo Mkuu wa Idara ya michezo Bw. Masoud Gumbwa ameweka wazi kuwa mashindano hayo yanayojumuisha michezo mbalimbali ikiwemo mpira wa miguu, mpira wa pete, mpira wa kikapu, mpira wa wavu pamoja na kuvuta ni maandalizi kwa ajili ya mashindano ya SHIMUTA ambayo yanatarajiwa kufanyika mapema mwezi Novemba, 2020 Jijini Tanga.



## MAKAMPUNI YASHAURIWA KUJITOKEZA KUDHAMINI MICHEZO SUA.



*Afisa michezo Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro Bi. Asteria Mwang'ombe akiongea wakati wa hafla ya kufunga rasmi michuano ya Chibunda Cup*

Makampuni mbalimbali ya kibiashara yameshauriwa kujitokeza katika kudhamini michezo Vyuoni hususani Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) ikiwa ni njia moja wapo ya kujitangaza na kuimarisha mahusiano baina ya makampuni hayo na Taasisi mbalimbali za Kielimu nchini.

Hayo yamesemwa na Afisa michezo Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro Bi. Asteria Mwang'ombe akimuwakilisha Mkurugezi wa Michezo Manispaa ya Morogoro wakati akifunga rasmi mashindano ya michezo ya ndani ya Wafanyakazi wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo maarufu kama "PROF. CHIBUNDA CUP" siku ya Ijumaa Tarehe 13 Novemba, 2020 kwenye viwanja vya michezo vya Kampasi ya Edward Moringe Mjini Morogoro.

Amesema kuwa licha ya michezo kuimarisha afya na kuburudisha miongoni mwa Wanajumuiya katika Taasisi husika, lakini pia inawaleta watu karibu na kufahamiana na hivyo kujenga mahusiano mazuri baina yao ikiwemo na jamii inayoizunguka kwa ujumla.

"Nimefarijika sana kusikia jitihada mbalimbali zinazofanywa na Chuo hiki kwa kushirikiana na wadau wengine zikiwemo taasisi za kifedha kama benki ya CRDB katika kuendeleza michezo Chuoni. Hongereni sana na nazidi kuwatia moyo katika kuendeleza juhudi hizi kwa nguvu kubwa ili kujiimarisha kimahusiano miongoni mwa jumuiya ya Chuo" alisema Bi. Asteria.

Awali akimkaribisha Mgeni rasimi kwa niaba ya Makamu Mkuu wa Chuo Prof. Raphael Chibunda, Naibu Makamu Mkuu wa Chuo kwa upande wa Utawala na Fedha, Prof. Amandus Muhairwa alimshukuru Mgeni rasimi kwa kuweza kuja kwa ajili ya kufunga rasimi mashindano hayo yaliyoanza Tarehe 9 Oktoba, 2020 licha ya majukumu aliyo nayo hasa katika kipindi hiki ambacho nchi imetoka katika uchaguzi mkuu.

Prof. Muhairwa pia alitumia fursa hiyo kuishukuru Benki ya CRDB kwa kuendelea kudhamini michezo chuoni hapo kwa kipindi cha miaka mine kitendo kinachoendelea kuipa thamani michezo na kuimarisha mahusiano baina ya Wanajumuiya wa SUA huku akiwakaribisha rasimi wadhamini wapya wa mashindano hayo Benki ya NMB.

Amesema kuwa lengo kubwa la mashindano hayo na mengine yanayofanyika Chuoni ni kuwakutanisha Wafanyakazi, kufahami-

*Inatoka Uk. 9*

ana, kuburudika, kuibua viapaji na kuimarisha afya lakini kubwa zaidi mashindano hayo hutumika kama maandalizi kwa ajili ya mashindano mbalimbali ya Kitaifa na Kimataifa kama vile SHIMUTA, Michezo ya Vyuo Vikuu vya Tanzania, Michezo ya Vyuo Vikuu vya Ulimwengu kwa Wanafunzi pamoja na Mabonanza mbalimbali yanayofanyika ndani na nje ya nchi.

"Ndugu Mgeni rasimi hivi leo timu zetu za mpira wa miguu pamoja na mpira wa pete zilizopo hapa uwanjani zianatarajia kusafiri siku ya kesho Tarehe 14 kuelekea Tanga ili kutuwakilisha katika michezo ya SHIMUTA " alisema Prof. Muhairwa

Amesema katika kuendeleza michezo chuoni, Chuo kimeendelea kuboresha miundombinu ya michezo, ikiwemo ujenzi na ukarabati wa viwanja na kununua vifaa vya michezo.

Wakiongeza kwa nyakati tofauti wawakilisha wa Benki za CRDB pamoja na NMB wameahidi kuendeleza ushirikiano wa karibu uliopo baina yao na Chuo cha SUA katika kuendeleza michezo pamoja na shughuli nyingine katika Chuo hicho.




***Afisa michezo Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro Bi. Asteria Mwang'ombe akisalimiana na wachezaji wa mpira wa miguu kabla ya kuanza kwa mchezo husika***

# VYUO VIKUU NCHINI VIMETAKIWA KUZALISHA WANAFUNZI WABUNIFU NA WAZALENDO



*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Uwekezaji) Prof. Kitila Mkumbo*

Vyuo Vikuu Nchini vimetakiwa kuzalisha wanafunzi wabunifu na wazalendo ambao wataweza kwenda kubuni miradi mbalimbali ambayo itawawezesha kujiajiri na kuajiri wengine ili kuweza kutatua changamoto ya upatikanaji wa ajira nchini pindi wanapohitimu masomo yao ya elimu ya juu.

Kauli hiyo imetolewa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Uwekezaji) Prof. Kitila Mkumbo wakati akizungumza katika mkutano Mkuu wa Mwaka wa Majalisi Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) Siku ya Alhamisi tarehe 17 Desemba 2020 ambao umeambatana na utoaji wa zawadi kwa wanafunzi wahitimu 211 ambao wamefanya vizuri katika masomo yao.

Prof. Mkumbo amesema kwa sasa nchi inahitaji vijana wabunifu na wazalendo ambao watakuwa chachu katika kuwekeza katika miradi mbalimbali ikiwemo ya kilimo ,ufugaji, na uvuvi huku akiweka msisitizo kwa vyuo vikuu nchini kuwa na utaratibu wa kuwaandaa vijana katika kuwafundisha zaidi namna ya kujiajiri pasipo kusubiri ajira kutoka serikalini.

"Lazima tubadilike kwenye ufundishaji wetu na tujue wanafunzi wanasoma nini ,kwa sasa dunia imebadilika tunahitaji vijana wanaoweza kujiajiri kwa hiyo sisi kama taasisi inayotoa elimu lazima tuwaandae vijana wetu zaidi kwenye kwenda kujiajiri, tukiweza kufanya hivyo na vijana wetu wakaelewa basi taifa letu litaondokana na changamoto ya ukosefu wa ajira" alisema Prof. Kitila Mkumbo

Kwa upande wake Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo upande wa Taaluma Prof. Maulid Mwatawala amesema SUA ni miongoni mwa vyuo ambavyo vinawaandaa wanafunzi zaidi kwenye kujiajiri na kuse-

*Inatoka Uk. 11*

ma kuwa SUA itakuwa mfano wa kuigwa nchini.

"Mhe. Waziri nikuakikishie tuko vizuri, wanafunzi wote wanaosoma masuala ya kilimo, mifugo, uvuvi na masuala ya utalii hawa wote tunawaandaa ili waweze kujiajiri"alisema Prof. Maulid Mwatawala

Katika mkutano Waziri wa Nchi,Ofisi ya Rais (Uwekezaji) Prof.Kitila Mkumbo amemkabidhi Mwanafunzi Musa Gese Doto tuzo mbili tuzo ya Mbunifu Bora wa Teknolojia ambapo amebuni gari shamba tuzo ambayo imetolewa na SETO TV na tuzo ya mbunifu bora wa Mwaka 2020 ambayo imetolewa na Tanzania Universities and Colleges Students Awards




***Mwanafunzi Musa Gese Doto wa SUA kutoka Idara ya Uhandisi Kilimo akiwa kwenye moja ya gari shamba alilobuni***



*Baadhi ya wageni waalikwa waliojitokeza kwenye mkutano mkuu wa mwaka wa Majalisi uliofanyika kwemye ukumbi wa Multpurpose uliopo Kampasi ya Edward Moringe, SUA Disemba, 2020*

# WAHITIMU SUA WATAKIWA KUTAMBUA HAKUNA KAZI YA MAISHA BALI KUNA FURSA ZA MAISHA



*Mwenyekiti wa Baraza la Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo SUA Mhe. Jaji Mstaafu Mohamed Chande Othman akiongea wakati wa Mahafali ya 36 ya Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) yaliyofanyika Disemba 18, 2020 kwenye Ukumbi wa Nelson Mandela Freedom Square, Mazimbu, Morogoro*

Wahitimu wa Chuo kikuu cha Sokoine cha Kilimo SUA wametakiwa kubadili fikra zao katika karne hii ya 21 kwa kutambua kuwa kwa sasa hakuna kazi ya maisha na badala yake waelewe kuwa kuna uhakika wa fursa za maisha ambazo ni nzuri na wanatakiwa kuzidaka kwa maendeleo yao na Taifa kwa ujumla .

Wito huo umetolewa na Mwenyekiti wa Baraza la Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo SUA Mhe. Jaji Mstaafu Mohamed Chande Othman, katika mahafali ya 36 ya Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo SUA yaliyofanyika Siku ya Ijumaa tarehe 18 Desemba 2020 katika ukumbi wa Nelson Mandela Freedom Square uliopo Kampasi ya Solomon Mhalangu Mazimbu SUA. akiwataka wahitimu hao wakatumie elimu waliyoipata katika kujenga taifa lao, na wakawe wenye nidhamu na waadilifu katika kazi zao za kila siku.

…"Kwa Karne hii ya ishirini na moja hakuna kazi ya maisha bali kuna fursa za maisha hivyo tumieni fursa mlizozipata vizuri mkalijenge taifa na kupeperusha bendera ya SUA." Alisema Jaji Mohamed Chande Othman.

Pia Jaji Mstaafu Mhe. Mohamed Chande Othman la Chuo ameishukuru Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ruzuku na fedha za maendeleo inayotoa kwa Chuo cha SUA ambazo ni dhahiri bila fedha hizo Chuo kisingeweza kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi uliofiki-

*Inatoka Uk. 13*

wa ikiwemo kuwa na idadi ya wahitimu 2943 kwa mwaka 2020.

Vile vile Mwenyekiti wa Baraza amebainisha kuwa Chuo kimeweza kutekeleza majukumu yake makuu kwa ufanisi mkubwa kwa kuisimamia Menejimenti ya Chuo ili itimize majukumu makuu ya Chuo hicho ambayo ni kutoa mafunzo, kufanya utafiti, kutoa huduma za kitaalamu na ugani pamoja na kuzalisha mali.

Kwa upande wake Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo SUA Prof. Raphael Chibunda ameeleza kuwa, katika Mahafali ya mwaka huu 2020 Wahitimu wa Kike wameongezeka kwa asilimia 25.5, ambapo Jumla ya wahitimu wa Kike kwa mwaka 2020 ni 1097 ambao ni sawa na asilimia 37.3, tofauti na wahitimu wa mahafali ya mwaka 2019 idadi ya wahitimu wa kike walikuwa 874.

Prof. Chibunda amesema kuwa ni ukweli usiofichika kuwa Chuo cha SUA kimekuwa ni Chuo ambacho kinapika wahitimu ambao kwa hakika shule wanayoipata sio ya lelemama wanatarajia wahitimu hao kuleta mafanikio ambayo yatakuwa kichocheo cha ufanisi, tija na ubunifu katika shughuli mbalimbali za ujenzi wa taifa ikiwemo kuzalisha mali na kutoa huduma bora kwa jamii na Taifa kwa ujumla.

"Mheshimiwa Mkuu wa Chuo, Kwa kutambua kwamba kusoma na kufikia hatua ya kutunikiwa cheti katika Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo haijawahi kuwa lelemama niombe ridhaa yako ya kuungana na Mwenyekiti wa Baraza la Chuo kuwapongeza kwa dhati watunukiwa wote kwa juhudi zao katika masomo ambazo zimewawezesha kufikia mafanikio waliyoyapata."Alisema Prof. Chibunda

Ameongeza kuwa wanawatarajia wahitimu wawe mabalozi wa kukitangaza Chuo vizuri kwa tabia na utendaji wao mzuri wa kazi, na kuwa ni mategemeo ya Chuo kwamba watatumia elimu waliyopata kuwa wabunifu, wajasiriamali na kuzalisha ajira zao wenyewe wakijiepusha kuwa wazururaji na walalamikaji.

Akieleza kuhusu udahili kwa mwaka wa masomo 2019/2020, Prof. Chibunda amesema chuo kimesajili jumla ya wanafunzi 5127 wapya wa shahada za kwanza, Stashahada na Atashahada ambao na tayari wameanza masomo, ambao kati yao, 4869 ni wa Shahada za kwanza, na 258 ni wa Stashahada na Astashahada, na kwa upande wa uzamili yaani wanafunzi wanaochukua masomo ya Umahiri na Uzamivu Chuo kimesajili jumla ya wanafunzi 151, hii inafanya kuwa na idadi ya wanafunzi wapya hadi tarehe 14 Desemba, 2020 ni 13,552.

Kwa upande wa Kampasi Mpya ya Mizengo Pinda iliyopo katika Kijiji cha Kibaoni, Wilaya ya Mlele Mkoa wa Katavi, ambayo Chuo kimeanzisha, kwa mwaka huu Chuo kimedahili wanafunzi 103 ambao wamesajiliwa na kuanza masomo katika katika programu tatu ambazo ni Shahada ya kwanza ya Sayansi ya Usimamizi Rasilimali Nyuki (BSc. Bee Resources Management), Stashahada ya Uzalishaji na Usimamizi wa Mimea Vipando (Diploma in Crop Production and Management) na Astashahada ya Uongozaji Watalii na Uwindaji Salama (Certificate in Tour Guiding and Hunting Operations).





# RAIS WA MAJALISI AHAIDI KUBORESHA BONANZA LA MICHEZO SUA



*Washiriki wa Bonanza wakishindana katika mchezo wa kusukuma kete maarufu kama Drafti, wakati wa Bonanza la Majalisi lilifanyika Kampasi ya Edward Moringe, SUA*

Rais wa Majalisi wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) Prof.Ludovic Kazwara kutoka Ndaki ya Tiba ya Wanyama na Sayansi za Afya SUA amehaidi kuboresha Bonanza la michezo ya Majalisi kwa mwaka 2021 ili ushiriki uwe mkubwa zaidi.

Ameyasema hayo wakati akifunga Bonanza la michezo ya Majalisi na kutoa zawadi kwa washindi walioshiriki kwenye michezo hiyo iliyofanyika Siku ya Jumatano tarehe 16 Novemba 2020 kwenye viwanja vya michezo vya Edward Moringe Kampasi Kuu SUA.

"Kuna baadhi ya michezo haikuchezwa mwaka huu sababu zilizo nje ya uwezo wetu lakini mwakani tutajiandaa mapema na kuongeza michezo mingi zaidi pia tutahakikisha ushiriki unakuwa mpana zaidi" amesema Prof. Kazwara.

Prof. Kazwara amesema kuwa lengo la michezo ya Majalisi ni kuwakutanisha pamoja Wahitimu na Wafanyakazi wa SUA na kuwajenga uhusiano mzuri kupitia michezo mbalimbali kama mpira wa Miguu, Mpira wa Pete, Mpira wa Kikapu, kuvuta Kamba, riadha, kukimbia kwenye magunia, drafti, kurusha tufe na kucheza karata.

Naye Mratibu wa michezo hiyo Dkt. Beda John Mwang'onde ambaye ni Mhadhiri Mwandamizi kutoka Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo SUA amesema kuwa Bonanza la michezo ya Majalisi linafanyikaga mara moja kwa mwaka kwa ajili ya kuwakaribisha tena Chuoni Wahitimu wa SUA katika Chuo hicho.

"Mwaka huu muitikio wa kushiriki kwenye michezo haukuwa mzuri sababu mambo yamekuwa mengi na yameongozana kwa pamoja hasa ukizingatia tupo mwishoni mwa mwaka watu wengi wameenda kwenye majukumu ya Chuo na ya Kitaifa" amesema Dkt. Mwango'mbe.

Lakini pia amewapongeza baadhi ya Majalisi na Wafanyakazi wa SUA waliotoa muda wao kwa kushiriki kwenye michezo hiyo kwani michezo ni Afya, michezo ni furaha na michezo ni burudani.

"kwa mwaka huu tumepata washiriki wazuri kama Prof. Elliot Phiri ambaye kwa umri wake tusingetarajia kumuona akikimbia mbio za mita 100 na kushika nafasi ya pili hatukutegemea kabisa hawashinde vijana kwenye mbio hizo" amesema Dkt. Mwango'mbe.

Akitoa neno la Shukrani Makamu wa Rais wa Majalisi Dkt. Raymond J. Salanga ambaye ni Mhadhiri kutoka SUA amewapongeza Majalisi, wafanyakazi na Wanafunzi kwa kujitoa kushiriki kwenye michezo hiyo ya Majalisi pamoja kuwa na majukumu mengine lakini waliona umuhimu wa kushiriki



***Baadhi ya Washiriki wa Bonanza wakiwa kwenye magunia tayali kwa ajili ya kushindana kukimbia***

***Inatoka Uk. 15***

wenye michezo hiyo.

“Tunakubali kuwa mwaka huu wa 2020 hatukuwa vizuri kama mwaka jana tuombe radhi kwenye mapungufu  yaliyojitokeza ni sababu zilizo nje ya uwezo wetu lakini tunahaidi kujipanga vizuri mwaka 2021” amesema Dkt. Salanga.

Bonanza la michezo ya Majalisi SUA ni jumuiko kuu la Alumni wote wa SUA ambalo hufanyika mara moja kwa mwaka, wiki moja kabla ya kutunuku shahada kwa wahitimu wa shahada za awali hadi uzamivu, maarufu kwa jina la "HOMECOMING WEEK". Ni Jumuiko na sehemu pekee muhimu inayowakutanisha wanazuoni, wafanyakazi na wahitimu wa SUA mwanzoni mwa mwaka wa masomo wakishiriki michezo mbalimbali na kufurahi pamoja.



***Baadhi ya Washiriki wa Bonanza wakiwa tayali kwa ajili ya kushindana kuvuta kamba***

# SUA YATAKIWA KUONGEZA KASI YA UTOAJI ELIMU KWA VITENDO IKIWEMO KUBORESHA MITAALA YAKE.



*na Mkurugenzi wa Idara ya Sayansi Teknolojia na Ubunifu kutoka Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia Prof. Maulilio Kipanyula akiongea katika halfa ya kutoa zawadi kwa wanafunzi wahitimu SUA waliofanya vizuri iliyofanyika Siku ya Alhamisi tarehe 17 Desemba 2020 kwenye ukumbi wa Multipurpose Kampasi ya Edward Moringe.*

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) kimetakiwa kuongeza kasi ya utoaji elimu kwa vitendo ikiwemo kuboresha mitaala yake ya ufundishaji ili kuwafanya wanafunzi wanaohitimu katika chuo hicho kujiajiri na kuajiri wengine.

Hayo yamebainishwa na Mkurugenzi wa Idara ya Sayansi Teknolojia na Ubunifu kutoka Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia Prof. Maulilio Kipanyula ambaye amemwakilisha Katibu Mkuu Wizara ya Elimu Sayansi na Tekinolojia Dkt. Reonald Akwilapo katika halfa ya kutoa zawadi kwa wanafunzi wahitimu SUA iliyofanyika Siku ya Alhamisi tarehe 17 Desemba 2020 kwenye ukumbi wa Multipurpose Kampasi ya Edward Moringe.

Prof. Kipanyula amesema kuwa muda muafaka umefika kwa chuo cha SUA kuangalia mitaala inayotumika kufundishia ili iweze kulenga zaidi kwenye kujiajiri.

“Ni wakati muafaka sasa kupunguza idadi ya wahitimu ambao wanamaliza na kuwaza kwenda kutafuta kazi duniani bali mitaala lazima iwawezeshe wahitimu waweze kujitegemea na kuzalisha ajira kujiajiri wenyewe na waaajiri watu

***Inatoka Uk. 17***

wengine " alisema Prof. Maulilio Kipanyula.
Prof. Kipanyula ameongeza kuwa Serikali itaendelea kuweka mazingira wezeshi ili kuvisaidia vyuo vikuu nchini viweze kuendelea kuzalisha wataalamu ambao wataweza kulisaidia taifa katika sekta mbalimbali ikiwemo ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi.
Kwa upande wake Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo SUA Prof. Raphael Chibunda amesema wanafunzi waliofanya vizuri na kupewa zawadi ni 211 ambao wametoka katika Ndaki na vitivo mbalimbali chuoni hapo ikiwemo wanafunzi bora wa mwaka ambao ni 195 pamoja na Idara sita bora ambazo zimefanya vizuri kwa kuchapisha katika tovuti
Prof. Chibunda amesema Chuo kitaendelea kutoa zawadi kwa wanafunzi wahitimu waliofanya vizuri kila mwaka katika masomo ili kutambua jitihada wanazofanya nwanafunzi hao ikiwa ni motisha ili wengine nao wafanye vizuri zaidi.

Naye mwanafunzi Bw. Iddy Msangi wa mwaka wa pili katika masomo ya sayansi ya kilimo , ambaye alipata tuzo , alisema hiyo ni motisha kwake ya kuendelea kupambana zaidi katika kuongeza bidii kwenye masomo yake.
"Namshukuru mwenyezi Mungu masomo yalikuwa magumu ila ni kwa uwezo wake Mungu nimekuwa miongoni mwa wanafunzi bora wa mwaka niwashauri wanafunzi wenzangu tunapokuwa chuoni tusome kwa bidii zaidi" alisema Idi Msangi

Kwa upande wake mwanafunzi, Upendo Nzaligo, wa mwaka wa pili katika masomo ya Uandaaji na Uwasilishaji wa taarifa ambaye alipata tuzo ya Sh 100,000 , alisema ameipokea kwa mikono miwili na itampatia fursa nzuri kujitangaza na inatamwongezea kuongeza juhudi katika masomo yake.



***Mkurugenzi wa Idara ya Sayansi Teknolojia na Ubunifu kutoka Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia Prof. Maulilio Kipanyula (wa pili, kushoto) akikabizi tuzo kwa mmoja wa wanafunzi wahitimu wa SUA waliofanya vizuri KWENYE MASOMO YAO , wakati wa Mkutano Mkuu wa mwaka wa Majalisi uliofanyika Kampasim Kuu ya Edward Moringe, SUA Disemba, 2020. Wa kwanza kushoto ni Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo Prof. Raphael Chibunda.***

# JAJI MSTAAFU, OTHMANI CHANDE AITAKA SUA KUTAFUTA NAMNA YA KUONGEZA VYANZO VYA MAPATO



*Mwenyekiti wa Baraza la Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) Jaji Mstaafu Mhe. Othmani Chande (mwenye nywele nyeupa) akiwa kwenye shamba darasa kitengo cha ufugaji Samaki, wakati wa ziara yake, SUA*

Mwenyekiti wa Baraza la Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) Jaji Mstaafu Mhe. Othmani Chande ameitaka SUA kutafuta namna ya kuongeza vyanzo vya mapato ya ndani ili kujiendesha

Akizungumza na Baadhi ya Watendaji wa Idara na Vitengo mbalimbali vya uzalishaji, Jaji Chande alisema kuwa mbali na kuwa jukumu kubwa la Chuo ni kufundisha na kufanya tafiti bado kuna nafasi kubwa ya kuzalisha mapato ya ndani.

Aidha aliongeza kuwa ni wakati wa Chuo kuangalia kama kinaridhika na mapato ya ndani yanayokusanywa kutoka vyanzo mbalimbali ama shughuli zinazofanyika ili kuleta mapato yan ndani

Nao Wakuu wa Idara na vitengo mbalimbali vya uzalishaji walipata fursa ya kueleza fursa mbalimbali ambazo zinapatikana SUA ikiwemo kuboresha maeneo ya kufanyia mikutano, kuwa na hospitali ya wanyama inayotembea ili kuwafikia wadau mbalimbali, kutengeneza madawa asilia pamoja na kuboresha sehemu mbalimbali zinazoweza kutumika kwa ajili ya shughuli za kitalii kama vile Morning Site pamoja na Botanical Garden.

Mwenyekiti huyo wa Baraza pia alipata fursa ya kutembelea maeneo mbalimbali ya Chuo ikiwemo Maktaba ya Taifa ya Kilimo (SNAL), Maabara ya TEHAMA, Shamba la mafunzo, pamoja na shamba la mafunzo (kitengo cha ufugaji Samaki)



**"ARDHI NI HAZINA"**

# HABARI PICHA ZA MATUKIO MBALIMBALI




*Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) Jaji Mstaafu Mhe. Joseph Sinde Warioba akipata maeleezo kushusu Maabara inayotembea ya inayomilikiwa na Hospitali ya Taifa ya Rufaa ya Wanyama, SUA kutoka kwa mmoja wa wataalam wa tiba za Wanyama.*



*Mwwenyekiti wa Baraza la Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) Jaji Mstafu Mhe. Othmani Chande (wa kwanza kulia) akipata maelezo toka kwa msimamizi wa Shamba darasa la mfano, Bw. Alpha Mtakwa alipotembelea shamba hilo wakati wa ziara yake ya siku mbili, SUA*



*Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) Jaji Mstaafu Mhe. Joseph Sinde Warioba akimtunuku shahada mmoja wa wanafunzi wakati wa Mahafali ya 36 ya Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) yaliyofanyika kwenye ukumbi wa Nelson Mandela Freedom Square, Mazimbu, Morogoro, Disemba, 2020*



*Mkurugenzi wa Idara ya Sayansi Teknolojia na Ubunifu kutoka Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia Prof. Maulilio Kipanyula (wa pili, kushoto) akikabizi tuzo kwa mmoja wa wanafunzi wahitimu wa SUA waliofanya vizuri KWENYE MASOMO YAO , wakati wa Mkutano Mkuu wa mwaka wa Majalisi uliofanyika Kampasim Kuu ya Edward Moringe, SUA Disemba, 2020.*



*Timu ya wavula ya wanafunzi wa SUA ikipasha misuli moto kabla ya kuanza kwa Bonanza la Majalisi*



*Mmoja wa washiriki katika Mkutano Mkuu wa mwaka wa Majalisi, SUA akichangia mada*

**"ARDHI NI HAZINA"**

# CHUO KIKUU CHA SOKOINE CHA KILIMO

**Imetolewa na:**
**Idara ya Mawasiliano na Masoko**
**SUA**

**S.L.P. 3000 CHUO KIKUU, MOROGORO,**
**TANZANIA**
**Simu: 255-023-2640006/7/8/9,**
**Barua pepe: communicationandmarketing@sua.ac.tz**



**"ARDHI NI HAZINA"**